UKUMBAKUMBA KATIKA SHERIA ZA FAMILIA YA KISALVATORIANI NA VYANZO VYAKE KWA BABA JORDANI

Janet E. Bitzan, SDS

18 June 2015

Wasalvatoriani kwa asili yao ni kumbakumba. Mpango maalumu wa awali uliotengenezwa na Baba Jordani, ulioitwa 'Rasimu ya Smyrna, Baba Jordani (1880) alielezea juu ya tabia kumbakumba ya Jamii Fundishi ya Kitume. Lengo la Jamii hii, aliandika Baba Jordani lilikuwa lina wajibu wa kujitakatifuza mtu binafsi na pia kusaidia "kila kiumbe kinachofikiri kiweze kufahamu juu ya Mungu wa kweli na Yeye aliyemtuma, Yesu Kristo…" Leo, Jamii ya Baba Jordani inaundwa na familia ya Wasalvatoriani – Mapadre, Mashemasi, Watawa Wanaume na wanawake na Walei ambao wamejiunga kwa pamoja kuendeleza "kazi ya Yesu ya kujitoa sadaka ili kutoa wokovu kwa viumbe vyote na ukombozi kutoka hatari na kupata uzima ulio kamilika (Sheria, aya, 10). Wazo la kuleta wokovu kwa ulimwengu mzima ni moja ya mambo matatu (3) muhimu ya tabia ya Wasalvatoriani ambayo inafahamika kama "ukumbakumba." Kwa Wasalvatoriani, ukumbakumba ni wito wa kuwahudumia watu wote, pamoja na watu wote ambao wameitwa kushiriki karama na utume wa Wasalvatoriani, na kwa njia na jinsi zote ambazo wanafunuliwa na Mungu.

Ukumbakumba kama wito wa kuwahudumia watu wote

Wakati ambapo Baba Jordani alikuwa akitayarisha rasimu kwa ajili ya jamii yake, alisali, "Ee Bwana wangu na mungu wangu, kwa msaada wako nisaidie kufanya jambo hili kwa ajili ya heshima yako, ili kila mmoja ajazwe na mafundisho yako matakatifu…" (Kumbukumbu ya Kiroho (SD) I 120). Jamii hii, alisisitiza, itakuwa "jamii ya Kikatoliki ya wenye daraja na watumishi katika shamba la Bwana ulimwenguni kote (SDI 124). Baada tu ya kuthibitishwa kwa Katiba ya Jamii yake mwaka 1886, Baba Jordani aliandika, "sadiki, amini, tumaini, penda na wajibika – wapeleke wote kwa Kristo. Ana deni kwa wote, kwa mataifa yote wanayotoka" (SD 192). Wasalvatoriani ni lazima watoke kati ya watu wote, kati ya mataifa yote, ili kila mmoja amjue kristo na kanisa lake.

Tunatimiza ukweli wa Milele wa neno wa Mungu na Imani yetu iweze kuwafikia watu wa kila tamaduni, kabila, tabaka, kundi la jamii, taifa na dini

Sheria # 8C

Kwa kufuata mfano wa Baba Jordani, Wasalvatoriani wa kipindi hiki wanamtangaza Yesu Kristo kwa "ulimwengu wenye hitaji la Mungu" (Sheria ya Familia, Aya 1). Tunaaswa 'tusipumzike mpaka watu wote duniani wamjue, wampende na wamtukuze Mungu' (Utangulizi, sheria ya Familia). Wazo la kutopumzika linaonyesha utume wetu ni wa kuchosha. Lakini, kazi aliyoifanya Baba Jordani kwa ajili ya utukufu wa Mungu haikuwa ngumu au ya

kuumiza. Toka mwanzo Baba Jordani alitambua ya kwamba kazi inayojihusisha na kuokoa roho za watu ni kazi inayozidi kazi zote kwa sababu ni kushiriki kazi ya ukombozi ya Mwokozi. Alimnukuu Dionysius Mwaaripago, Myunani au Mwanafalsafa na Mwanatauhidi wa Kisiria (500 AD). Ambaye alieleza juu ya wazo hili, "jambo la Kimungu kuliko mambo yote matakatifu ni kufanya kazi pamoja na Mungu kwa ajili ya wokovu wa watu" (SD 199). Wajibu wowote unaofanywa kwa nia njema, ulimpa Baba Jordani furaha ya roho, faraja na amani ya roho (SD 134) na raha (SD I 138).

Ukumbakumba kama Wito wa Kuhudumia Watu Wote

Rasimu ya Smyrna (1880) ilifafanua muundo wa asili wa madaraja matatu (3) ya Jamii Fundishi ya Kitume. Daraja la kwanza lilikuwa linaundwa na Mapadre wote wa Kanuni za Kikatoliki, Masista na Wakristo Walei ambao kwa hiari yao, kama mitume, walijitolea wazimawazima kufanya kazi kwa ajili ya jamii. "Hawa wanachama walipewa jukumu la kufundisha mashule na seminari za wakazi katika maeneo yao…Ambapo utukufu wa Mungu utahitaji utume huo." Kundi la pili linaundwa na Wataalam na wasomi, makleri na walei, ambao wana utaalamu wao na wanabaki katika majukumu yao. "kundi hili lilipewa wajibu wa wanaobaki katika majukumu yao." Kundi hili lilipewa wajibu wa "kukuza na kueneza elimu na mafunzo ya Kikatoliki kadri ya uwezo wao…" na hatimaye, kundi la tatu linaundwa na Walei waume na Walei Wanawake. Walei hawa walipewa majukumu ya "kuwatunza watoto waliokabidhiwa kwao" na kuhakikisha kwamba watoto hawa wanapatiwa "malezi na elimu bora ya Ukatoliki."

Mwaka 1883, Baba Bonaventura Luthen, rafiki wa karibu sana wa Baba Jordani, aliandika "katika kipindi chetu, kuliko kipindi kingine chochote kila mmoja wetu ni lazima asaidie kazi za kuokoa roho. Kila mmoja afanye hilo popote alipo na kwa njia yoyote awezayo – lakini ni lazima afanye kitu! Na kwa yeyote yule anayependa kujiunga nasi, tunawaalika kwa mikono miwili kama ndugu zetu katika urafiki wa kiroho, tukimwomba Mungu Mwenyezi pamoja na malaika wake awabariki na kuimarisha urafiki huu (Mmisionari, # 7). Kila mmoja alikuwa na nafasi katika jamii hii mpya.

Katika moja ya kazi zake nzuri, Ukumbakumba kama upendo kwa wote…, Sr.Carol Thresher (1997) alisema kwamba uanachama wa mwanzo kabisa wa Jamii Fundishi ya Kitume, "inaonyesha jinsi muono wake [Baba Jordani] ulivyomuhusisha kila mmoja…kilichokuwa muhimu kwake ilikuwa ni jitihada na moto katika moyo wa hawa mitume. Utaifa, jinsia, tabaka, hadhi ya kanisa, au asili ya mtu ilikuwa ni kitu cha ziada." (Uk. 65 – 66) Kama Baba

"Kama Familia ya Kisalvatoriani, tunahitaji kutoa ushuhuda unaoonekana kwa waume na wake kutoka katika tamaduni na historia mbalimbali ikifanya kazi kuendana na utume. Tunaboresha uaminifu na heshima kwa tofauti tulizonazo, tunajifunza kutoka kwa kila mmoja, na kuthamini mambo yote yanayotusaidia katika maisha na utume wetu."

Sheria # 14

Jordani alivyowaandikia wanachama wake siku ya Jumapili ya Matawi, 1913, “Jamii ambayo imekusudiwa kwa ajili ya watu wote ina deni kwa wote. Kwa hiyo, muwahusishe watu wote katika upendo wenu wa kila tabaka au taifa” (ilinukuliwa kutoka Cerltty, 1988, uk. 88). Ilivyouundwa kwa kufuata muono wa asili wa Baba Jordani, Jamii Fundishi ya Kitume, ilikuwa na madaraja matatu kufuatana na jinsi kila kundi linavyojihusisha na utume wa jamii, jamii hii ilidumu kama kwa mwaka mmoja hivi. Baba Jordani kwa sababu maalumu alibadili jamii hii Fundishi kuwa Shirika la Kitawa (kwa wanaume) mwezi machi, 1883” (schommer 1992, uk. 183) na kwa wakati huohuo alianzisha kisheria shirika la wanawake. Uanachama wa Walei, ambayo idadi ya wanachama wake ilikuwa haifahamiki kwa kundi la kwanza na la pili na “zaidi ya wanachama 1000 katika kundi la tatu (3) (Skwor, 1993 uk. 219) lilikuwa hai mpaka lilipotokea katika mfumo tofauti mwaka 1971. Mfumo huu mpya ndio kundi la Wasalvatoriani Walei wa familia ya Kisalvatoriani.

Wanachama wa familia ya Kisalvatoriani katika karne ya 21inaundwa na mapadre, mashemasi, watawa wa kiume, watawa wa kike na wakristo walei. Wanachama walei ni wanaume na wanawake wenye ndoa au wasio na ndoa. “Tunaishi wito wetu kwa usawa na kuheshimu tofauti zetu mbalimbali zinazosababishwa na hali ya maisha, karama na tamaduni (sheria, aya ya 4).

“tunafanya jitihada ya kutoa utume wazi wa wanaume na wanawake kutoka katika tamaduni na mazingira tofauti tukifanya utume wetu kwa pamoja. Tunajifunza kuamini na kuheshimu tofauti zilizopo kati yetu, kujifunza kutoka kwa kila mmoja na kuthamini mchango ambao kila mmoja anaweza kutoa kwa ajili ya utume na maisha yetu. (sheria aya, 14)

Ukumbakumba unajionyesha katika tofauti ya uanachama wetu na hali ya ukarimu ilivyoenea na mwaliko wetu kwa watu wanaoishi katika parokia na taasisi za Kisalvatoriani na taasisi mbalimbali zinazopenda kujiunga nasi katika utume. Kwa kufuata mfano wa waanzilishi wetu, tunakubaliana “na wito kwa wabatizwa wote kuwa ni msukumo unaoishi katika kanisa na kwa ulimwengu wa haki…” (sheria, sura 7).

Ukumbakumba kama wito wa kutumia njia na namna zote

Kama tulivyoona mipango ya mwanzo ya Baba Jordani kwa jamii pamoja na uanachama wa familia ya Kisalvatoriani. Kwa leo ina watu wa nyakati zote na mitindo yote ya maisha, wanafanya kazi kwa pamoja kutimiza utume. Baba Pancratius Pfeiffer (1919), Mkuu wa pili wa Jamii ya Wasalvatoriani, alibaini kwamba lilikuwa ni lengo la Baba Jordani kutoka mwanzo kumtukuza Mungu na kumfanya ajulikane kwa watu wote na pia kwa kutumia njia na namna zote.

Awali katika Kumbukumbu ya Kiroho, Baba Jordani alijishauri ya kwamba, “kwa njia yoyote ile inayowezekana jiue mwenyewe na uishi kwa ajili ya Mungu peke yake” (SD I 21). Na, ingawa alikuwa Yerusalemu, alikusudia “kufanya haraka inavyowezekana kufanya kazi yote iliyokusudiwa na Mungu,” (SD 152a). Baba Jordani aliandika “tumia njia yoyote halali iliyopo” (SD I 53a). Katika toleo la kwanza la Mmisionari, Baba Luthen aliandika “tunaikubali njia yoyote halali: sayansi na sanaa, elimu na utume, machapisho na jamii na kwa namna yoyote ndani mwetu

tunatamani kusaidia kuboresha mambo yote haya, ili tuweze kuwawezesha tena watu kuwa na ari takatifu kwa imani na fadhila" (Pfeiffer, 1930, uk. 81).

Baadae, alipokuwa akiandika katiba ya Jamii ya Mungu Mwokozi, baba Jordani aliwaelekeza wanachama kutumia "njia na jinsi zote ambazo zitaongozwa na upendo wa Kristo" kumtukuza na kumfanya Mungu ajulikane, kumsifu Mama wa Mungu na kuokoa roho zote." (Pfeiffer, 1919 uk. 3). Baba Pfeiffer alionyesha ya kwamba Baba Jordani aliona ukumbakumba wa njia na namna yoyote kuwa jambo muhimu na tabia ya kijamii. "Pingamizi lolote lilikuwa ni kitu kigeni kwake (Baba Jordani) na lilikuwa ni jambo lisilozoeleka kwa jamii ya Mungu Mwokozi". (Pfeiffer, 1919, uk. 3).

Kiuhalisia kulikuwa na pingamizi moja lililokuwa juu ya namna mbalimbali katika huduma za Kisalvatoriani. Tunatakiwa kutumia tu zile njia ambazo wataangaziwa na upendo wetu kwa Mungu. "Roho yetu ya Ukumbakumba inajionyesha kwa njia na namna yoyote ambazo zitaangaziwa na upendo wa Mungu. (aya ya 8). Baba Pfeiffer alituthibitishia kwamba upendo wa Mungu utatuonyesha "namna nzuri" na kwa hiyo, Wasalvatoriani "tunaweza kutumia njia yoyote ile tunayoweza, kwa kutilia maanani uwezekano wowote ule uliopo mbele yetu." (Pfeiffer, 1919, uk. 4)

Mwaka 1920, ambapo baadhi ya wanachama, walikuwa wakiuliza uwezekano wa Mapadre Wasalvatoriani waache kufanya utume mashuleni, Baba Pfeiffer alifafanua kwamba uamuzi kuhusiana na namna gani nzuri ipewe kipaumbele na itumike kwa muda uliopo, inategemea na mazingira – kama uchaguzi wa dawa kwa ajili ya ugonjwa. "Ni lazima tukubali kwamba, kwa sasa, baada ya vita kuu ya kwanza na madhara yake makubwa ulimwenguni, watu wamechanganyikiwa na wanahitaji sana kushtuliwa, hii inaweza ikafanyika, kama ilivyo thibitishwa, kwa namna maalumu kupitia utume wa maparokia. Kwa hiyo kwa muda huu, kwa ushauri wetu inaonekana kuwa ni njia bora na inayohitajika sana". (Pfiffer, 1920, uk. 25) Kifungu hiki kinaonyesha kwamba Baba Pfeiffer alielewa utume mbalimbali ambao unaweza kufanywa katika mazingira tofauti na ya Kihistoria. Ukumbakumba utawawezesha Wasalvatoriani kukubaliana na kile ambacho mara kwa mara kinaitwa "alama za nyakati"

Baada ya miaka, Baba Leornard Gerke alisema kwamba watoto wa Baba Jordani, "wakusudie na wawe tayari kufanya jambo lolote, kutumia jinsi yoyote, kutumia njia yoyote ambayo upendo wa Wokovu wa Kristo utawaongoza, na ambao, mazingira yake yataonyeshwa na maongozi ya Mungu." (Gerke1965, uk. 12). Wazo kama hilo lilitolewa na Sr. Miriam cerlety (1997) katika makala yake, njia na namna zozote, "zawadi ya njia na namna yoyote ni lazima ithaminiwe na iheshimiwe. Haiwezekani kufafanuliwa katika ukamilifu wake. Inahitaji kuwa na maono ya sala" (Uk. 4). Ukumbakumba wa njia na namna unaonyesha kwamba Wasalvatoriani wanatumia rasilimali na karama na vipaji vya watu binafsi kwa muono mbalimbali wa namna tofauti. Sala na utambuzi inawaangazia na kutoa mwelekeo kwa matendo ya Kisalvatoriani.

Hitimisho

Ukumbakumba ni tabia ya kudumu ya Wasalvatoriani. Unaweza ukagundua vyanzo vya ukumbakumba katika kazi mbalimbali binafsi alizoandika Baba Jordani na pia katika dokumenti maalumu za awali za Jamii ya Wasalvatoriani kutokana na sababu hii, mitindo mbalimbali za ukumbakumba imeingizwa katika sheria ya sasa ya familia ya Wasalvatoriani. Wasalvatoriani wanahudumia watu wote, karibu na mbali, kufanya watu wote wamjue Mungu mmoja wa kweli na Yesu Kristo, ili wao na wale wanaowatumikia wawe na uzima wa milele. Wasalvatoriani wanatimiza utume huu kama "familia moja ya mitume waliojitolea ambao wanawatangazia wote utukufu ambao unaonekana kwa Yesu Kristo." (Tito 3:4, kama ilivyonukuliwa katika sheria, aya ya 3.)

Maswali ya Tafakari

1. Soma tena Sheria za Familia ya Kisalvatoriani kwa mwanga wa makala hii.
    a. Onyesha maneno au misemo ambayo inakugusa na ujiulize, "jambo hili linaniambia mimi nini na nitalipa mwitikio gani?"
    b. Manufaa yake yanaweza kuwa ni yapi katika familia ya Kisalvatoriani katika eneo lako la ulimwengu au/na kwa ulimwengu mzima?
2. Kwa mwanga wa makala hii, kama ukiamua kuitengeneza upya sheria ya familia ya Wasalvatoriani, Je, Utaongeza kitu gani au kukibadili?
3. Nina uzoefu gani wa kipekee wa Ukumbakumba? Uzoefu huu una mchango gani katika kukua kwangu kiroho?
4. "Kufanya kazi kwa Mungu kwa ajili ya Wokovu wa Watu" (Baba Jordani). Leo hii ina maana gani kwangu/kwetu? Ninaweza kutafsiri vipi kwa lugha ya kisasa?